



**JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA  
WIZARA YA MAJI**



**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA  
MAZINGIRA MUSOMA**

MKATABA WA AJIRA YA KAZI YA UPASUAJI WA MAWE YENYE JUMLA YA  
MITA ZA UJAZO 375

KATI YA

BW. SAMWEL NYAZORO

NA

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUSOMA

(MUWASA)

MRADI WA UPANUZI WA MTANDAO WA MAJI KWENDA KATIKA MITAA  
SABA ISIYOPATA HUDUMA YA MAJI

Makubaliano ya Upasuaji wa mawe kwenye uchimbaji wa mtaro wa kulaza bomba kuu la kusafirisha maji kutoka Kata ya Kwangwa hadi Kata ya Bweri Manispaa ya Musoma yamefanyika leo tarehe 14 Machi 2022 kati ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) S.L.P 233 MUSOMA (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mlipaji")

Na

Bw. **Samwel Nyazoro** (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mpasua Mawe")

Ambapo Mpasua Mawe tajwa hapo juu atafanya kazi ya kupasua mawe katika mtaro wa kulaza bomba kuu kuanzia mtaro unapoanzia katika kata ya Kwangwa hadi Kata ya Bweri. Mpasua Mawe atahakikisha mawe yaliyopasuliwa yanatolewa kwenye mtaro hadi hapo msimamizi wa mradi atakapohakikisha ulazaji wa bomba linalazwa pasipo kikwazo chochote cha kuzuiwa na mawe. Gharama ya Upasuaji wa mawe kwa kila mita moja ya ujazo ni Shilingi za Tanzania Elfu Ishirini (20,000/=) tu na gharama hii inahusisha vitendea kazi vyote vinavyohitajika wakati wa Upasuaji wa mawe kama ilivyoaninishwa katika jedwali hapa chini: -


Na.	Aina ya Kazi	Kizio	Idadi	Kiasi	Jumla
1	Upasuaji wa mawe	m <sup>3</sup>	375	20,000/=	7,500,000/=
Jumla kuu					<b>7,500,000/=</b>

Malipo ya Mpasua mawe yatalipwa kupitia akaunti namba **NMB 30610018857**

Makubaliano haya yameshuhudiwa na: -

**Kwa Niaba ya Mwajiri:**


Jina: Mhandisi Nicas Mgisha

Sahihi: 

Cheo: Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

**Shahidi**

Jina: Mhandisi Burton Kajigili

Sahihi: 

Cheo: Kaimu Meneja Ufundi

**Mwajiriwa:**

Jina: Samwel Nyazoro

Sahihi: 

Cheo: Mpasua mawe

**Shahidi**

Jina: JOHN MARIWA

Sahihi: 

Cheo: KIBARUA